

Language: Swahili

Kumkumbuka Ngũgĩ wa Thiong’o: Shujaa wa Kifikra na Fasihi Kutoka Afrika

Paul M. MUKUNDI

Department of English and Language Arts,
Morgan State University, Baltimore, USA

E-mail: paul.mukundi@morgan.edu

ORCID iD <https://orcid.org/0000-0001-6759-4120>

IKISIRI

Makala hii inamrejelea upya Ngũgĩ wa Thiong’o kama msomi wa Kiafrika mwenye ushawishi mkubwa zaidi kwa uandishi wa kifasihi ambao unaingia katika nadharia ya kisiasa, falsafa ya ukoloni mamboleo, na taaluma pana za ubinadamu. Kwa kumweka wa Thiong’o ndani ya muktadha wa kihistoria wa ukoloni, mapambano ya kupinga ukoloni na hata hali ya Afrika baada ya uhuru, makala hii inafuatilia jinsi mkondo wa fikra zake—kuanzia fasihi yake ya msingi hadi ile ya ukosoaji mkali wa lugha na utamaduni—unavyounda changamoto endelevu dhidi ya mifumo ya maarifa ya kikoloni. Kwa kutumia mbinu ya kiuchambuzi ya kitafsiri inayojengwa juu ya historia ya fikra, uhakiki wa fasihi ya baada ya ukoloni, na nadharia ya kuondoa ukoloni, utafiti huu unaunganisha usomaji wa karibu wa matini na uwekaji wa kazi katika muktadha wake wa kihistoria ili kuchunguza maendeleo na umuhimu wa urithi wa kifikra wa Ngũgĩ wa Thiong’o. Kwa usomaji wa kina wa maandishi yake kama vile riwaya, insha, na maandiko yake ya kinadharia inadhihirika kuwa mchango wake mkubwa unapatikana katika namna anavyofafanua lugha kama eneo la mamlaka, kumbukumbu, na upinzani. Aidha, maandishi haya yanachunguza jinsi uhamisho wake kutoka Afrika ulivyounda upya maendeleo yake kama msomi wa kimataifa, na hivyo kumwezesha kuukosoa ukoloni mamboleo kama mfumo unaodumishwa kupitia utamaduni, elimu, na uzalishaji wa maarifa. Kupitia uchambuzi wa kazi zake za baadaye za kifasihi, makala hii pia inaonyesha kwamba maandishi ya wa Thiong’o yanatangulia nadharia za kisasa za ukoloni mamboleo huku yakibaki yamejikita katika uzoefu wa kihistoria wa Afrika. Mwisho, makala hii inathibitisha kuwa mwandishi huyu ni shujaa wa kimaadili na kiakili ambaye dhamira yake kwa haki ya lugha, uhuru wa kitamaduni, na uwajibikaji wa kisiasa inaendelea kuathiri mijadala katika fasihi na tafiti za baada ya ukoloni.

Relembrando Ngũgĩ wa Thiong’o: um herói do pensamento e da literatura da África

Este artigo reexamina Ngũgĩ wa Thiong’o como um intelectual africano fundamental, cuja influência transcende a produção literária e alcança a teoria política, a filosofia decolonial e o campo mais amplo das humanidades. Situando wa Thiong’o na trajetória histórica que abrange o colonialismo, a luta anticolonial e a desilusão do pós-independência, o ensaio descreve como sua trajetória intelectual — desde a ficção nacionalista inicial até a crítica linguística e cultural radical — constitui um desafio constante às epistemologias coloniais. Empregando uma metodologia interpretativa fundamentada na história intelectual, na crítica literária pós-colonial e na teoria decolonial, o estudo combina a análise textual detalhada com a contextualização histórica para examinar a evolução e a relevância do legado intelectual de wa Thiong’o. Com base em leituras atentas de seus romances, ensaios e escritos teóricos, este artigo

argumenta que a contribuição central de wa Thiong’o reside na sua articulação da linguagem como um espaço de poder, memória e resistência. O texto examina, ainda, como o exílio reformulou sua formação intelectual global, possibilitando uma crítica da colonialidade enquanto sistema transnacional sustentado pela cultura, pela educação e pela produção de conhecimento. Por meio da análise de sua ficção mais recente, o ensaio argumenta também que a obra de wa Thiong’o antecipa a teoria decolonial contemporânea, mantendo-se, contudo, ancorada na experiência histórica africana. Por fim, o artigo apresenta o escritor como uma figura heroica, tanto no plano ético quanto no intelectual, cujo compromisso com a justiça linguística, a soberania cultural e a responsabilidade política continua a moldar os debates nos campos da literatura e dos estudos pós-coloniais.

Remembering Ngũgĩ wa Thiong’o: An African Intellectual and Literary Hero

ABSTRACT

This article reconsiders Ngũgĩ wa Thiong’o as a foundational African intellectual whose influence extends far beyond literary production into political theory, decolonial philosophy, and the broader humanities. Situating wa Thiong’o within the historical arc of colonialism, anticolonial struggle, and post-independence disillusionment, the essay traces how his intellectual trajectory—from early nationalist fiction to radical linguistic and cultural critique—constitutes a sustained challenge to colonial epistemologies. Employing an interpretive methodology grounded in intellectual history, postcolonial literary criticism, and decolonial theory, the study combines close textual analysis with historical contextualization to examine the evolution and significance of wa Thiong’o’s intellectual legacy. Drawing on close readings of his novels, essays, and theoretical writings, this article argues that wa Thiong’o’s central contribution lies in his articulation of language as a site of power, memory, and resistance. The paper further examines how exile reshaped his global intellectual formation, enabling a critique of coloniality as a transnational system sustained through culture, education, and knowledge production. Through an analysis of his later fiction, the essay further argues that wa Thiong’o’s work anticipates contemporary decolonial theory while remaining grounded in African historical experience. Ultimately, the article positions the writer as an ethical and intellectual hero whose commitment to linguistic justice, cultural sovereignty, and political responsibility continues to shape debates across literature and postcolonial studies.

MBINU YA UTAFITI

Utafiti huu unatumia mbinu ya kiubora ya kiuchambuzi inayojengwa juu ya historia ya fikra, uhakiki wa fasihi ya baada ya ukoloni, na nadharia ya kuondoa ukoloni. Badala ya kutoa wasifu kamili wa kihistoria wa Ngũgĩ wa Thiong’o, makala haya yanafanya uchambuzi wa kina wa kazi zake kuu za kifasihi, za tawasifu, na za kinadharia, ili kufuatilia maendeleo ya fikra zake na ushawishi wake katika nyanja za fasihi, siasa, historia, na taaluma za ubinadamu. Mbinu ya usomaji wa karibu wa matini inatumika kuchunguza kwa kina kazi zake, kazi hizi zikiwa *Weep Not, Child* (Usilie Mwanangu), *A Grain of Wheat* (Punje ya Ngano), *Petals of Blood* (Petali za Damu), *Devil on the Cross* (Shetani Msalabani), *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African literature* (Kuondoa Ukoloni Akilini: Siasa za Lugha katika Fasihi ya Kiafrika), *Moving the Centre: The Struggle for Cultural Freedoms* (Kusogeza Kituo: Mapambano ya Uhuru wa Kitamaduni), *Writers in Politics: Essays* (Waandishi katika Siasa: Insha), *Globalectics: Theory and the Politics of Knowing* (Globalectics: Nadharia na Siasa za Kujua), na *Wizard of the Crow* (Mchawi wa Kunguru). Uchambuzi huu umewekwa ndani ya miktadha mipana ya kihistoria ya ukoloni, mapambano dhidi ya ukoloni, ujenzi wa taifa baada ya uhuru, na maisha ya uhamishoni.

Aidha, utafiti huu unategemea tafiti za hivi karibuni katika taaluma za fasihi ya baada ya ukoloni, nadharia ya kuondoa ukoloni, uhakiki wa fasihi ya Kiafrika, na taaluma za ubinadamu wa kimazingira, ili kutathmini jinsi mawazo ya wa Thiong’o yalivyofasiriwa, kukosolewa, na kuendelezwa katika mijadala ya kisasa ya kitaaluma. Kwa kuunganisha uchambuzi wa wasifu, uwekaji wa kazi zake katika muktadha wa kihistoria, na usomaji wa karibu wa maandishi yake, utafiti huu unamchukulia wa Thiong’o si tu kama mwandishi wa fasihi, bali pia kama msomi mkuu wa Kiafrika ambaye mchango wake unaangazia mijadala endelevu kuhusu lugha, utamaduni, mamlaka, uzalishaji wa maarifa, na uondoaji wa ukoloni.

Utangulizi: Ngũgĩ wa Thiong’o na Historia ya Kifikra ya Kuondoa Ukoloni

Ngũgĩ wa Thiong’o (1938–2023) anasimama kama mmoja wa wasomi wenye athari kubwa zaidi waliotokea katika Afrika ya karne ya ishiringi. Katika taaluma iliyochukua zaidi ya miongo sita, alizalisha kazi nyingi zinazovuka mipaka ya riwaya, tamthilia, tawasifu, uhakiki wa fasihi, na nadharia ya kisiasa, huku zote zikisalia kuunganishwa na dira thabiti ya kimaadili na kifalsafa. Zaidi ya kuwa mwandishi wa riwaya au mchangiaji wa mijadala ya kitamaduni, wa Thiong’o anashika nafasi ya kipekee kama mwananadharia wa kuondoa ukoloni, ambaye maandishi yake yanachunguza kwa kina athari za urithi wa ukoloni hasa kisaikolojia, kiisimu, na kimuundo. Mwelekeo wa fikra zake unaakisi mkondo wa kihistoria wa Afrika baada ya ukoloni—kuanzia matumaini ya uhuru, kupitia usaliti uliotekelezwa na viongozi wa Kiafrika, ukandamizaji wa tawala za kimabavu baada ya ukoloni, hadi uhamisho wa mwandishi huyu alikoendeleza shughuli zake za mapambano yanayohusu haki ya kimaarifa.

Hata hivyo, mazoea ya kifasihi ya wa Thiong’o hayawezi kutenganishwa na dhamira yake ya kisiasa na kimaadili iliyoendelea kwa uthabiti. Kupitia kazi zake, anasisitiza kwamba fasihi si chombo kisichoegemea upande wowote; kwa mtazamo wake, uandishi ni tendo la kijamii lililojikita katika mahusiano ya mamlaka. Kama anavyosema kwa uwazi, “Literature cannot escape from the class power structures that shape our everyday life” (Fasihi haiwezi kuepuka miundo ya mamlaka ya kitabaka inayounda uhalisia wa maisha ya kila siku) (wa Thiong’o, 1986a, uk. 3). Kwa mantiki hiyo, uzalishaji wa fasihi ni chombo kinachoshirikiana na mifumo ya utawala au nyenzo ya upinzani dhidi yake.

Katika miongo miwili iliyopita, tafiti za kitaaluma zimeanza kumtambua wa Thiong’o si tu kama mwandishi mashuhuri wa Kiafrika bali pia kama msomi wa msingi katika mijadala ya kimataifa kuhusu kuondoa ukoloni. Ukosoaji wake wa ubeberu wa lugha, unaobainika sana katika *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature* (Kuondoa Ukoloni Akilini: Siasa za Lugha katika Fasihi ya Kiafrika, 1986), umekuwa kiini cha mijadala kuhusu haki ya maarifa, elimu baada ya ukoloni, na fasihi duniani kote. Wakati huo huo, kazi zake za kifasihi—hasa *A Grain of Wheat* (Punje ya Ngano, 1967), *Petals of Blood* (Petali za Damu, 1977), na *Wizard of the Crow* (Mchawi wa Kunguru, 2006)—zinaendelea kusomwa kama uchunguzi wa kina wa migongano ya kimaadili baada ya ukoloni. Bila tashwishi, maandishi haya yanamweka Ngũgĩ wa Thiong’o kama shujaa wa fasihi ya Kiafrika ambaye ushawishi wake unaenea zaidi ya fasihi na kuingia katika fikra za kisiasa, historia, na taaluma pana za ubinadamu. Urithi wake wa kudumu hauko tu katika alichandika, bali pia katika namna alivyoifafanua upya nafasi na wajibu wa msomi wa Kiafrika katika ulimwengu wa baada ya ukoloni.

Uundaji katika Wakati wa Ukoloni na Uelewa wa Kihistoria

Ngũgĩ wa Thiong’o alizaliwa mwaka 1938 huko Limuru, katika Nyanda za Juu za kati za Kenya, wakati ambapo utawala wa kikoloni wa Uingereza ulikuwa umefikia

kilele chake cha ukandamizaji na unyonyaji. Sera za ardhi za kikoloni zilisababisha kuondolewa kwa sehemu kubwa ya jamii ya Wakikuyu kutoka ardhi zao, na kuwalazimisha kuingia katika ajira za kulipwa au kuishi katika maeneo yenye msongamano mkubwa. Serikali ya kikoloni ilisimika mfumo wa ubaguzi wa rangi kupitia sheria, elimu, na matumizi ya nguvu, na hivyo kuunda mpangilio wa kijamii uliotegemea unyang’anyi wa Waafrika. Ufahamu wa kisiasa wa wa Thiong’o ulianza kujengeka ndani ya mazingira haya.

Katika *Dreams in a Time of War: A Childhood Memoir* (Ndoto za Wakati wa Vita: Tawasifu ya Utotoni, 2010), wa Thiong’o anatafakari jinsi utawala wa kikoloni ulivyofanya kazi si tu kupitia ukandamizaji wa kimwili bali pia kupitia uundaji upya wa fahamu. Shule za wamisionari, licha ya kutoa ujuzi wa kusoma na kuandika, zilikuza pia hali ya kujitenga na utamaduni wa mtu binafsi. Watoto Waafrika walifundishwa kuhusisha utamaduni wa Ulaya na akili pamoja na maendeleo, huku lugha na tamaduni zao wenyewe zikionyeshwa kama za nyuma na zisizo na thamani. wa Thiong’o (1986a) anakumbuka kwamba elimu ya kikoloni ilihitaji “the deliberate disassociation of the child from his cultural base” (kitendo cha makusudi cha kumtenganisha mtoto na msingi wake wa kitamaduni) (uk. 17). Uzoefu huu ulisababisha kwa wa Thiong’o mpasuko wa kisaikolojia ambao baadaye ungekuwa msingi wa kazi yake ya kinadharia.

Aidha, uasi wa *Mau Mau* wa miaka ya 1950 uliathiri kwa kiasi kikubwa mtazamo wa wa Thiong’o kuhusu dunia. Hata ingawa hakuwa mpiganaji, alishuhudia moja kwa moja ukatili wa ukandamizaji wa kikoloni: kufungwa kwa watu wengi, mauaji, kuhama kwa kulazimishwa, na uharibifu wa vijiji. Uzoefu huu ulifichua uwongo wa dhana kwamba ukoloni ulikuwa wa huruma, na kuonyesha wazi kwamba mamlaka ya kikoloni yalitegemea hofu na vurugu. Katika kazi zake za baadaye, wa Thiong’o alirudia mara kwa mara kipindi hiki, akikionyesha kama wakati wa upinzani wa kishujaa lakini pia wa mgongano wa kimaadili.

Athari za *Mau Mau* zinaonekana wazi katika *A Grain of Wheat* (Punje ya Ngano, 1967), ambamo mapambano ya ukombozi hayaonyeshwi kama simulizi rahisi ya wema dhidi ya uovu, bali kama eneo la usaliti, kujitolea, na hatia zisizotatuliwa. Kukataa kwa riwaya hii kutoa taswira ya kishujaa isiyo na shaka kunaakisi utambuzi wa mapema wa wa Thiong’o kwamba uhuru, ingawa ulikuwa muhimu, haukuweza peke yake kutatua migongano iliyozalishwa na ukoloni.

Vilevile, wa Thiong’o aliathiriwa kwa kina na mila za simulizi za mdomo za Wakikuyu. Hadithi, methali, nyimbo, na maonyesho ya kijamii yalitoa mfumo mbadala wa maarifa uliotegemea kumbukumbu za pamoja na mafunzo ya kimaadili. Mila hizi ziliunda si tu mtindo wake wa uandishi bali pia dira yake ya kisiasa. Hata kabla ya kuanzisha nadharia yake ya kuondoa ukoloni wa lugha, wa Thiong’o alikuwa ameshaanza kuelewa kwa kina kwamba utamaduni haupitishwi tu kupitia maandishi, bali pia kupitia mazoea ya kijamii yanayohifadhi utambulisho wa jamii yoyote.

Mwanzo wa Kazi ya Kifasihi na Kipindi cha Utaifa

Kazi za awali za riwaya za Ngũgĩ wa Thiong’o ziliibuka katika kipindi cha mabadiliko makubwa ya kisiasa. Uhuru wa Kenya katika mwaka 1963 ulizua matumaini makubwa, ukiambatana na mijadala yenye msisimko kuhusu utambulisho wa taifa, uhuishaji wa utamaduni, na maana halisi ya uhuru. Ni katika mazingira haya ya kihistoria yenye msukumo mkubwa ndipo wa Thiong’o alichapisha *Weep Not, Child* (Usilie Mwanangu, 1964), riwaya ya kwanza kubwa kwa lugha ya Kiingereza kutoka kwa mwandishi wa Afrika Mashariki.

Riwaya hii inaakisi matarajio pamoja na migongano ya utaifa wa awali. Elimu inaonekana kama njia ya ukombozi, lakini pia inaonyeshwa kuwa chombo kinachoendeleza tabaka za kijamii zilizorithiwa kutoka kwa ukoloni. Unyang’anyi wa ardhi, ukosefu wa usawa wa kiuchumi, na migogoro ya vizazi inaenea katika simulizi,

ikidokeza kwamba uhuru haukuweza kuondoa dhuluma za msingi zilizotokana na utawala wa kikoloni. Kama anavyobainisha Simon Gikandi (2000), kazi za awali za wa Thiong’o tayari zinaonyesha “a profound unease with the moral foundations of nationalism itself” (msumbuko wa kina kuhusu misingi ya kimaadili ya utaifa wenyewe) (uk. 15).

Kwa upande mwingine, riwaya *The River Between* (Mto Ulioko Kati, 1965) inaendeleza ukosoaji huu kwa kuonyesha migogoro ya kitamaduni iliyosababishwa na uingiliaji wa kikoloni. Riwaya hii inaweka wazi mgongano kati ya Ukristo na mifumo ya imani za kienyeji, na hivyo kuonyesha jinsi usasa wa kikoloni ulivyogawanya jamii za Kiafrika. Badala ya kuwasilisha mila na usasa kama vitu vinavyopingana kabisa, wa Thiong’o anafichua ukatili uliomo katika kulazimisha mgawanyiko huo. Msiba wa riwaya hii hauko katika tofauti za kitamaduni zenyewe, bali katika mazingira ya kikoloni yaliyofanya muafaka uwe mgumu kufikiwa.

Kupitia *A Grain of Wheat* (Punje ya Ngano, 1967), wa Thiong’o alifikia hatua muhimu ya mafanikio ya kisanaa na kiitikadi. Riwaya hii inaacha mtindo wa simulizi ya moja kwa moja na ushujaa wa mtu binafsi, na badala yake inatumia sauti ya pamoja inayowakilisha ugumu wa uzoefu wa kihistoria. Ikiwa imewekwa katika mkesho wa uhuru, riwaya hii inachunguza kwa kina utata wa kimaadili wa mapambano ya ukombozi, ikionyesha usaliti, hofu, na maafikiano pamoja na ujasiri. Kwa kufanya hivyo, mwandishi anapinga simulizi za kitaifa zinazorahisisha mapambano ya uhuru kuwa hadithi zisizo na utata wa kishujaa.

Ingawa kazi hizi za awali ziliandikwa kwa Kiingereza, tayari zinaashiria kutoridhika kwa wa Thiong’o na lugha ya kikoloni. Ufahamu wake unaoongezeka kuhusu athari za kiitikadi za uchaguzi wa lugha hatimaye ulisababisha mojawapo ya mabadiliko makubwa zaidi katika historia ya fasihi ya kisasa.

Ubadilikaji wa Kisiasa, Tamthilia na Utamaduni wa Umma

Kufikia mwanzoni mwa miaka ya 1970, Ngũgĩ wa Thiong’o alikuwa ameanza kukata tamaa kuhusu hali ya kisiasa ya Kenya baada ya uhuru. Ahadi za uhuru na usawa zilikuwa zimegeuka kuwa ukandamizaji wa kisiasa, ukosefu wa usawa wa kiuchumi, na mkusanyiko wa madaraka mikononi mwa tabaka dogo la watawala. Kwa kujibu hali hii, maandishi yake yalichukua mwelekeo ulio wazi zaidi wa Kimarxisti na kupinga ukoloni mamboleo.

Mabadiliko haya yalijitokeza kwa uwazi zaidi kupitia ushiriki wake katika tamthilia za jamii huko Kamĩĩĩĩĩ. Tamthilia *Ngaahika Ndeenda* (*I Will Marry When I Want*) (Nitaoa Nitakapotaka, 1977), iliyoandikwa kwa lugha ya Gĩkuyu na kuigizwa na wakulima pamoja na wafanyakazi, iliwakilisha hatua kubwa ya kuachana na utamaduni wa kifasihi wa tabaka la juu. Tamthilia hii ilishughulikia moja kwa moja unyang’anyi wa ardhi, unyonyaji wa kitabaka, na usaliti wa maadili ya utaifa. Matumizi yake ya lugha ya Gĩkuyu na mbinu za maonyesho ya watu wa kawaida yalipinga dhana kwamba sanaa makini lazima iandikwe kwa Kiingereza na kulenga hadhira ya wasomi pekee.

Majibu ya serikali dhidi ya tamthilia hiyo yalikuwa ya haraka na yenye ukali mno. Mnamo Desemba 1977, wa Thiong’o alikamatwa bila kufikishwa mahakamani na kufungwa katika Gereza la Usalama wa Juu la Kamĩĩĩĩ. Tukio hili lilikuwa hatua ya mgeuko mkubwa katika maisha yake ya kifikra. Akiwa gerezani, wa Thiong’o aliamua kuacha kutumia Kiingereza kama lugha ya ubunifu, akitambua kwamba utawala wa lugha ulikuwa umefungamana moja kwa moja na ukandamizaji wa kisiasa. Kama alivyoandika baadaye, “The bullet was the means of physical subjugation. Language was the means of spiritual subjugation” (Risasi ilikuwa chombo cha kutiisha kimwili; lugha ilikuwa chombo cha kutiisha kiroho) (1986a, uk. 9).

Zaidi ya hayo, riwaya *Devil on the Cross* (Shetani Msalabani, 1980), aliyoandika kwa lugha ya Gĩkuyu akiwa gerezani, inasimama kama ushahidi wa mabadiliko haya.

Muundo wake wa kifumbo, mtiririko unaofanana na simulizi za mdomo, na ukosoaji mkali wa unyonyaji wa kibepari vinaakisi imani yake kibiliswamba fasihi lazima izungumze moja kwa moja na hali halisi ya maisha ya watu waliokandamizwa. Katika muktadha huu, uandishi wenyewe ukawa tendo la upinzani, na lugha ikawa uwanja wa mapambano ya kisiasa na kiutamaduni.

Lugha, Mamlaka, na Nadharia ya Kuondoa Ukoloni

Mchango wa kudumu na wenye athari kubwa zaidi wa Ngũgĩ wa Thiong’o katika fikra za kimataifa unapatikana katika namna alivyoendeleza nadharia kuhusu lugha kama eneo la mamlaka. Wakati waandishi wengi wa baada ya ukoloni walijadili mada ya kutengwa kitamaduni kwa njia ya kifasihi, wa Thiong’o aliwasilisha ukosoaji wa kimumo kuhusu jinsi utawala wa kikoloni unavyofanya kazi kupitia ngazi za lugha. Uingiliaji wake wa kifikra, uliobainishwa kwa kina zaidi katika *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature* (Kuondoa Ukoloni Akilini: Siasa za Lugha katika Fasihi ya Kiafrika, 1986), ulibadilisha mijadala katika taaluma ya fasihi ya Kiafrika na kuathiri kwa kiasi kikubwa majadiliano kuhusu elimu, maarifa, na uzalishaji wa utamaduni duniani kote.

Kiini cha hoja ya wa Thiong’o katika *Decolonising the Mind* ni msisitizo kwamba ukoloni huacha athari zake za kudumu zaidi, siyo tu katika mipaka ya kisiasa au mifumo ya utawala bali katika fahamu za watu. Anasema, “The domination of a people’s language by the languages of the colonizing nations was crucial to the domination of the mental universe of the colonized” (kutawaliwa kwa lugha ya watu na lugha za mataifa ya kikoloni kulikuwa muhimu katika kutawala ulimwengu wa kiakili wa waliotawaliwa) (wa Thiong’o, 1986a, uk. 16). Kauli hii inaeleza kiini cha hoja yake: kwamba utawala wa lugha huzalisha aina ya utengano wa kisaikolojia unaoendelea hata baada ya uhuru wa kisiasa kupatikana. Katika mtazamo huu, lugha huwa chombo ambacho kupitia kwake, maadili, ngazi za kijamii, na mitazamo ya kikoloni huingizwa ndani ya fikra za watu.

wa Thiong’o anaeleza mchakato huu kwa uwazi zaidi kupitia mfumo wa elimu ya kikoloni. Shuleni, watoto Waafrika waliadhibiwa kwa kuzungumza lugha zao za mama na kupewa motisha wanapotumia lugha za Ulaya. Kadiri muda ulivyopita, hali hii ilizalisha kile alichokiona kama utengano wa kikoloni ambapo watoto Waafrika walijifunza kuhusisha utamaduni wao wenyewe na aibu pamoja na hali ya nyuma, huku wakichukulia utamaduni wa Ulaya kama ishara ya akili na maendeleo. Anaandika kwamba mfumo huu “made the child see the world and where he stood in it as seen and defined by or reflected in the culture of the language of imposition” (ulimfanya mtoto auone ulimwengu na nafasi yake ndani yake kama unavyoonekana, kufasiliwa au kuakisiwa katika utamaduni wa lugha iliyolazimishwa) (wa Thiong’o, 1986a, uk. 17). Matokeo yake yalikuwa mgawanyiko wa kisaikolojia kati ya nafsi ya mtu na utamaduni wake, na kati ya fikra na uzoefu.

Muhimu zaidi, wa Thiong’o haichukulii lugha kama chombo cha mawasiliano tu. Kwa mtazamo wake, lugha hubeba utamaduni, kumbukumbu, na mifumo ya maarifa. Kama anavyoeleza, “Language carries culture, and culture carries, particularly through orature and literature, the entire body of values by which we come to perceive ourselves and our place in the world” (lugha hubeba utamaduni, na utamaduni hubeba—hasa kupitia fasihi simulizi na fasihi andishi—jumla ya maadili ambayo kupitia kwake tunajitambua na kuelewa nafasi yetu katika ulimwengu) (wa Thiong’o, 1986a, uk. 6). Kwa hivyo, kulazimisha lugha ya kigeni ni sawa na kulazimisha namna ya kigeni ya kuishi na kufikiri. Lugha za kikoloni, kwa mtazamo wake, hazikuwa tu zana za utawala—zilibadilisha kabisa namna Waafrika walivyojielewa na kuuelewa ulimwengu wao.

Hivyo basi, uamuzi wake wa kuandika hasa kwa lugha ya Gĩkuyu haukuwa kukataa uwepo wa lugha nyingi wala kupuuza mahitaji ya mawasiliano ya kimataifa. Badala yake, ulikuwa ni kukataa mfumo wa ngazi za lugha unaotukuza lugha za kikoloni kuliko lugha za Kiafrika. Kwa kufanya hivyo, wa Thiong’o alisisitiza kwamba lugha za Kiafrika zimekuwa zikinyimwa uhalali wa kiakili, na kwamba kuzirejesha katika matumizi ya kisomi na kifasihi ni hatua muhimu katika mradi wa kuondoa ukoloni.

Katika kazi yake ya baadaye *Globalectics: Theory and the Politics of Knowing* (*Globalectics: Nadharia na Siasa za Kujua*, 2012), wa Thiong’o anaendeleza wazo la “globalectics,” ambalo linafafanua maono ya utamaduni wa dunia unaotegemea mazungumzo badala ya utawala. Globalectics inapinga wazo la kituo kimoja cha kitamaduni ambacho maarifa husambazwa kutoka kwake kwenda pembezoni. Badala yake, inapendekeza ulimwengu ambapo lugha na tamaduni mbalimbali zinaingiliana kwa usawa. Mfumo huu wa kinadharia unapinga mitazamo ya kibeberu ya fasihi ya dunia na kutangulia mijadala ya kisasa inayosisitiza uwepo wa mifumo mingi ya maarifa.

Katika tafiti za hivi karibuni, mawazo ya wa Thiong’o yamezidi kutambuliwa kama msingi wa nadharia ya kuondoa ukoloni. Watafiti wamebainisha kwamba kazi zake zinatangulia ukosoaji wa baadaye kuhusu ukosefu wa usawa wa maarifa na ngazi za kimfumo za utawala wa fikra zinazohusishwa na wananadharia kama Aníbal Quijano (2000) na Walter Mignolo (2011). Tofauti na baadhi ya wanazuoni wanaokosoa ukoloni mamboleo huku wakibaki kutumia lugha za Ulaya pekee, wa Thiong’o aliendelea kujitolea kuandika, kutafsiri, na kuendeleza nadharia kwa lugha ya Gĩkuyu licha ya changamoto za kitaaluma. Kwa njia hii, mazoezi yake ya kifikra yalidhihirisha kwa vitendo misingi aliyokuwa akiitetea.

Uhamisho na Uundaji wa Kifikra wa Kimataifa

Uhamisho wa Ngũgĩ wa Thiong’o mwanzoni mwa miaka ya 1980 ulikuwa mojawapo ya nyakati muhimu zaidi katika maisha yake ya kifikra. Ingawa mara nyingi uhamisho huu umeelezwa kwa misingi ya wasifu—hasa kutokana na ukandamizaji wa kisiasa chini ya utawala wa Rais Daniel Moi—ni sahihi zaidi kuelewa kama hatua ya kupanuka kwa fikra iliyombadilisha kutoka mwandishi wa kitaifa hadi msomi wa kimataifa. Uhamisho ulimlazimisha wa Thiong’o kufikiria upya uhusiano wake na mahali, lugha, na mamlaka, na kwa kufanya hivyo uliimarisha uchambuzi wake wa ukoloni mamboleo kama mfumo wa kimataifa badala ya tukio la kihistoria lililojikita katika taifa moja.

Baada ya kukamatwa kwake mwaka 1977 na kuachiliwa baadaye, wa Thiong’o alijikuta akiwa chini ya ufuatiliaji na vitisho vya mara kwa mara. Kutorejeshwa katika nafasi yake ya kufundisha katika Chuo Kikuu cha Nairobi, pamoja na kukandamizwa kwa kazi zake za tamthilia, kulifanya iwe vigumu kwake kuendelea kuishi nchini Kenya. Kuondoka kwake mwaka 1982 hakukuwa kukimbia majukumu, bali uhamisho wa kulazimishwa—hali iliyowakumba wasomi wengi wa Kiafrika ambao ukosoaji wao wa tawala za baada ya ukoloni uliwafanya kuwa katika hatari za kisiasa. Hata hivyo, kwa wa Thiong’o, uhamisho haukusababisha kujitenga na siasa; badala yake, uliimarisha uelewa wake kuhusu jinsi mamlaka yanavyofanya kazi katika mipaka, taasisi, na mifumo ya fikra.

Akiwa uhamishoni, wa Thiong’o alipata fursa ya kushuhudia kwa karibu jinsi taasisi za kitaaluma za Magharibi zinavyoshughulikia maarifa ya Kiafrika—mara nyingi yakipangwa, kuainishwa, na hata kupunguzwa thamani ndani ya mifumo ya kimataifa ya maarifa. Uzoefu huu uliimarisha imani yake kwamba ukoloni haukuwa tukio la kihistoria lililopita bali hali endelevu ya kifikra. Kama alivyoandika, “Imperialism continues to control the economy, politics, and cultures of the formerly colonized

nations, but more importantly it controls the way people perceive themselves and the world” (Ubeberu unaendelea kudhibiti nyanja za uchumi, siasa, na utamaduni katika mataifa yaliyowahi kuwa chini ya ukoloni; lakini zaidi ya yote, unadhibiti namna watu wanavyojitambua na kuutambua ulimwengu) (wa Thiong’o, 1986a, uk. 89). Kwa mtazamo huu, uhamisho ulikuwa nafasi ya kipekee iliyomwezesha kuutazama ukoloni mamboleo kama mfumo wa kimataifa.

Katika kipindi hiki pia, wa Thiong’o alianza kufafanua kwa uwazi zaidi vipengele vya kimaadili vya upinzani wa kitamaduni. Kwa mtazamo wake, uhamisho haukupunguza wajibu wake bali uliuongeza. Umbali kutoka Kenya haukumwondolea dhamira ya kisiasa; badala yake, ulipanua upeo wa dhamira hiyo. Kazi yake ya kufundisha barani Ulaya na baadaye Marekani ilimuwezesha kushirikiana na jamii za Waafrika ughaibuni, wanafunzi, na wasomi waliokuwa wakikabiliana na maswali yanayofanana kuhusu utambulisho, lugha, na mamlaka. Mikutano hii ilizidi kuthibitisha imani yake kwamba utawala wa kitamaduni haujidhihirishi tu kupitia nguvu za dola bali pia kupitia taasisi za maarifa.

Aidha, tafakari za wa Thiong’o kuhusu uhamisho zinaunganishwa kwa karibu na ukosoaji wake mpana wa kutengwa kwa msomi na jamii yake. Mara kwa mara alionya dhidi ya hatari ya wasomi wa Kiafrika kujitenga na jamii zilizowalea. Katika *Moving the Centre: The Struggle for Cultural Freedoms* (Kusogeza Kituo: Mapambano ya Uhuru wa Kitamaduni, 1993), anatahadharisha kwamba uhamisho haupaswi kuleta “a condition of silence or accommodation,” (hali ya ukimya au maafikiano) bali unafaa kuwa “a space from which to challenge the structures that made exile necessary in the first place” (nafasi ambayo inamwezesha mtu kupinga miundo iliyosababisha uhamisho wa lazima) (wa Thiong’o, 1993, uk. 87). Msisitizo huu unatofautisha mtazamo wake na aina za mtazamo wa ughaibuni zinazosherehekea uhamaji huku zikisahau mizizi ya kisiasa ya hali hiyo.

Kuandika kwa lugha ya Gĩkuyu akiwa nje ya nchi pia kulikuwa tendo la makusudi la upinzani dhidi ya kile alichokiona kama nguvu za usawazishaji wa utamaduni wa kimataifa. Kama alivyosisitiza, “The choice of language and the use to which language is put is central to a people’s definition of themselves in relation to their natural and social environment” (uchaguzi wa lugha pamoja na matumizi yake ni kiini cha namna watu wanavyojitambua katika uhusiano wao na mazingira ya asili na kijamii) (wa Thiong’o, 1986a, uk. 4). Kwa hivyo, uhamisho uliigeuza lugha kuwa nguzo ya kisiasa na kimaadili, ukimuwezesha kudumisha uhusiano wa kitamaduni hata alipokuwa akihama kutoka sehemu moja ya dunia kwenda nyingine.

Muhimu zaidi, uhamisho ulimpa nafasi ya kuimarisha zaidi uchambuzi wake kuhusu ubepari wa kimataifa na ukoloni mamboleo. Alianza kuona tawala za kimabavu za baada ya ukoloni si kama hali za kipekee bali kama mwendelezo wa miundo ya kikoloni inayofanya kazi kupitia mbinu mpya. Kazi zake zilianza kusisitiza kwa nguvu zaidi jinsi taasisi za kifedha za kimataifa, mijadala ya maendeleo, na utandawazi wa kitamaduni zinavyoendeleza mifumo ya ubaguzi iliyorithiwa kutoka ukoloni.

Fasihi ya Baadaye na Kejeli ya Mamlaka ya Baada ya Ukoloni

Kazi za baadaye za kifasihi za Ngũgĩ wa Thiong’o zinaakisi kilele cha maendeleo yake ya kisiasa na kisanaa. Riwaya kama *Matigari* (1986) na *Wizard of the Crow* (Mchawi wa Kunguru, 2006) zinaonyesha mwelekeo kuelekea matumizi ya istiaara, kejeli, na mitholojia kama njia za ukosoaji wa kisiasa. Kazi hizi zinavuka mipaka ya istiaara ya kitaifa na kuingia katika uchambuzi wa vipengele vya kimataifa vya mamlaka ya baada ya ukoloni, zikifichua jinsi mantiki za kikoloni zinavyoendelea kupitia mifumo mipya ya utawala, utegemezi wa kiuchumi, na utawala wa kitamaduni.

Isitoshe, riwaya *Matigari* inachukua nafasi ya mpito katika kazi za wa Thiong’o. Riwaya hii, iliyoandikwa kwa lugha ya Gĩkuyu muda mfupi baada ya kuachiliwa kwake

kutoka gerezani, inamfuata mpiganaji wa uhuru anayerejea kutoka msituni akiwa na imani kwamba uhuru umeleta haki, lakini anagundua kwamba unyonyaji unaendelea chini ya watawala wapya. Sura ya Matigari inafanya kazi kama mhusika na pia kama ishara—ikiwakilisha ahadi ambazo hazikutimizwa za harakati za ukombozi barani Afrika. Kwa mtazamo wa wa Thiong’o, historia haijasonga mbele kwa mstari ulionyooka bali imejirudia kwa kuzaa mifumo ya zamani ya ukandamizaji katika sura mpya. Kudumu kwa ukosefu wa usawa kunaonyesha mipaka ya uhuru wa kisiasa ambao haujaambatana na mageuzi ya kimuundo. Hivyo, *Matigari* inaashiria kukumbatia kikamilifu kwa wa Thiong’o mbinu ya istiaara kama chombo cha kufichua migongano ya utawala wa baada ya ukoloni.

Mwelekeo huu unafikia upeo wake katika *Wizard of the Crow* (Mchawi wa Kunguru, 2006), riwaya pana na inayokiuka mipaka ya kijinsia za fasihi. Ikiwa imewekwa katika taifa la kubuni la Aburiria, riwaya hii inakejeli udikteta, misaada ya kigeni, fedha za kimataifa, na upuuzi wa tawala za kimabavu. Kupitia matumizi ya kuzidisha mambo kwa makusudi na vipengele vya uhalisia wa kichawi, wa Thiong’o anafichua asili ya maigizo ya mamlaka pamoja na ushirikiano wa taasisi za kimataifa katika kuendeleza tawala kandamizi.

Kiini cha *Wizard of the Crow* ni ukosoaji wa kile wa Thiong’o anakiita “theatre of power” (tamthilia ya mamlaka)—yaani, taratibu, maonyesho, na simulizi ambazo mamlaka hutumia kujihalalisha. Viongozi katika riwaya hii wamejikita katika hadhi, vyeo, na miradi mikubwa ya maendeleo isiyo na tija, huku wananchi wakiteseka chini ya umaskini wa kiuchumi. Hali hii inaakisi mifumo halisi katika mataifa ya baada ya ukoloni, ambapo lugha ya maendeleo ya kibepari hufunika ukosefu wa usawa wa kimuundo.

Aidha, *Wizard of the Crow* inachanganya kejeli ya kisiasa na mila za simulizi za mdomo. Riwaya hii inategemea muundo wa hadithi za jadi, usimulizi wa pamoja, na kumbukumbu za jamii ili kudhoofisha mamlaka ya simulizi rasmi. Kwa kufanya hivyo, wa Thiong’o anarejesha hadithi kama eneo la upinzani. Usimulizi unatumika kama chombo cha kufichua uongo, kuhifadhi historia, na kubuni uwezekano mbadala wa siku zijazo.

Ni muhimu pia kubainisha kwamba kejeli ya wa Thiong’o si ya kukata tamaa. Ingawa ukosoaji wake wa mamlaka ni mkali, umejengwa juu ya imani thabiti katika uwezo wa watu wa kawaida. Msisitizo wa riwaya hii juu ya uvumi, mitandao ya uvumi, na usimulizi wa pamoja unaonyesha imani yake katika hekima ya kisiasa ya wananchi. Kwa maana hii, *Wizard of the Crow* haiwakilishi kukata tamaa, bali inawakilisha upinzani—kukataa kuacha fikra huru itawaliwe na dhuluma.

Tathmini Mpya ya Kitaaluma ya Kisasa na Umuhimu wa Kinadharia

Tangu mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja, ushiriki wa kitaaluma na kazi za Ngũgĩ wa Thiong’o umepitia mabadiliko makubwa ya kimwelekeo. Wakati ukosoaji wa awali mara nyingi ulimweka kama mwandishi wa utaifa au wa Kimarxisti wa kipindi cha baada ya uhuru, tafiti za hivi karibuni zimeanza kumtambua kwa kiwango kikubwa zaidi kama mwananadharia wa msingi wa kuondoa ukoloni. Mabadiliko haya yanaakisi mageuzi mapana ndani ya taaluma za ubinadamu, hasa kuongezeka kwa msisitizo juu ya haki ya maarifa, ukosefu wa usawa wa kimataifa, na siasa za uzalishaji wa maarifa.

Miongoni mwa michango muhimu katika tathmini hii mpya ni kazi ya Brian Sibanda, *The Decolonial Politics and Philosophy of Ngũgĩ wa Thiong’o* (Siasa na Falsafa ya Kuondoa Ukoloni ya Ngũgĩ wa Thiong’o, 2024), ambayo inadai kwamba maandishi ya wa Thiong’o yanaunda mfumo thabiti wa kifalsafa badala ya kuwa mfululizo wa maingilio ya kifasihi yenye msukumo wa kisiasa pekee. Sibanda anamweka wa Thiong’o sambamba na wanazuoni wakuu wa nadharia ya kuondoa ukoloni, akisisitiza kwamba ukosoaji wake wa lugha, utamaduni, na mamlaka unatanguka mijadala ya kisasa

kuhusu ukoloni mamboleo kama muundo endelevu wa kimataifa. Kwa mujibu wa Sibanda (2024), mradi wa kifikra wa wa Thiong’o unatoa changamoto ya kifalsafa kwa mifumo ya maarifa inayozingatia Ulaya, kwa sababu unasisitiza uhalali wa lugha za Kiafrika kama vyombo vya nadharia na wala siyo tu vyombo vya utamaduni pekee (uk. 52).

Utambuzi huu unaashiria mabadiliko muhimu katika namna wa Thiong’o anavyosomwa. Badala ya kuzingatia insha zake kama nyongeza tu kwa kazi zake za kifasihi, watafiti sasa wanasisitiza kwamba maandishi yake ya kinadharia—hasa *Writers in Politics: Essays* (Waandishi katika Siasa: Insha, 1981), *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature* (Kuondoa Ukoloni Akilini: Siasa za Lugha katika Fasihi ya Kiafrika, 1986), na *Moving the Centre: The Struggle for Cultural Freedoms* (Kusogeza Kituo: Mapambano ya Uhuru wa Kitamaduni, 1993) — yanaunda mkusanyiko wa fikra unaoingilia moja kwa moja masuala ya maarifa, maadili, na mamlaka. Msisitizo wa wa Thiong’o kwamba lugha huunda namna tunavyoelewa ulimwengu unamweka karibu na wanazuoni wa baadaye wa nadharia ya kuondoa ukoloni kama Aníbal Quijano (2000), aliyebainisha dhana ya “coloniality of power” (uendelevu wa mamlaka ya kikoloni) (uk. 533) kama muundo unaoendelea kuathiri mifumo ya maarifa ya kisasa.

Kinachomtofausha wa Thiong’o ndani ya muktadha huu wa kifalsafa ni jinsi anavyounganisha nadharia na mazoezi ya kifasihi. Tofauti na wanazuoni wanaofanya kazi katika kiwango cha nadharia tupu, wa Thiong’o anajenga fikra zake kupitia simulizi, maonyesho, na uzoefu wa kihistoria. Riwaya zake, tamthilia, na tawasifu si mifano tu ya nadharia, bali ni maeneo ambamo nadharia hutengenezwa. Kama anavyobainisha Simon Gikandi (2000), kazi za wa Thiong’o “collapses the artificial distinction between creative writing and theoretical reflection,” (zinavunja mpaka bandia uliowekwa kati ya uandishi wa ubunifu na tafakuri ya kinadharia, na hivyo kuunda aina ya uzalishaji wa maarifa unaojikita katika mapambano ya kihistoria) (uk. 8).

Tafiti za hivi karibuni pia zimezidi kuangazia umuhimu wa mawazo ya wa Thiong’o katika mijadala ya kuondoa ukoloni katika elimu, hasa katika muktadha wa marekebisho ya mitaala na sera za lugha. Ukosoaji wake wa elimu ya kikoloni—hasa upendeleo wa lugha za Ulaya kama vyombo vya kipekee vya maarifa—umetumika katika mijadala ya taasisi mbalimbali barani Afrika na katika ulimwengu kwa ujumla. Kwa mfano, nchini Afrika Kusini, mageuzi ya mitaala baada ya ubaguzi wa rangi yameathiriwa na hoja za wa Thiong’o kuhusu jinsi ngazi za lugha zinavyoendeleza ukosefu wa usawa wa maarifa. Wanazuoni kama Neville Alexander (1989) wamependekeza, kwa kuafikiana na wa Thiong’o, kupanua matumizi ya lugha za Kiafrika kama vyombo vya kufundishia katika elimu ya juu ili kuwezesha usawa wa upatikanaji wa maarifa.

Aidha, mijadala kuhusu harakati za kuondoa ukoloni katika mitaala iliyo katika vyo vikiu kama vile Chuo Kikuu cha Cape Town na Chuo Kikuu cha Witwatersrand imeendelea kurejelea hoja ya wa Thiong’o kwamba “language carries culture” (lugha hubeba utamaduni) (wa Thiong’o, 1986a, uk. 16) ili kupinga utawala wa Kiingereza katika uzalishaji wa maarifa ya kitaaluma. Nje ya Afrika, ushawishi wake unaonekana pia katika mijadala ya elimu katika eneo la Karibiani, ambapo wanazuoni wanaojadili sera za lugha—hasa kuhusiana na lugha za Krioli—wametumia hoja za wa Thiong’o kuisitiza umuhimu wa kuthibitisha na kuhalalisha lugha za kienyeji ndani ya mifumo rasmi ya elimu. Kwa mfano, Hubert Devonish amependekeza matumizi ya Krioli ya Jamaica kama lugha halali ya kufundishia, akidai kwamba mifumo ya elimu inayotukuza lugha za kikoloni huzaa upya mifumo ya ukosefu wa usawa wa kitamaduni na kimaarifa (Devonish, 1986). Aidha, Carolyn Cooper ametetea kutambuliwa kwa Krioli ya Jamaica kama lugha halali ya uzalishaji wa maarifa na ubunifu wa kifasihi, akipinga ngazi za

kikoloni zinazoyapuuza na kuyadunisha maumbo ya lugha za kiasili (Cooper, 1995). Katika mazingira haya, kazi za wa Thiong’o zimekuwa si tu za ukosoaji, bali pia zimekuwa mfumo wa kufikiria upya elimu kama jumba la utofauti wa maarifa na uwajibikaji wa kitamaduni.

Zaidi ya hayo, wanazuoni kama Graham Huggan na Helen Tiffin (2010) wamechunguza vipengele vya kimazingira na kimaadili katika maandishi ya wa Thiong’o, wakimuweka ndani ya uwanja unaokua wa ekokritiki ya baada ya ukoloni. Kazi yao, hasa *Postcolonial Ecocriticism: Literature, Animals, Environment* (Ekokritiki ya Baada ya Ukoloni: Fasihi, Wanyama, Mazingira, 2010), inaonyesha jinsi maandishi ya baada ya ukoloni yanavyochunguza uhusiano kati ya unyonyaji wa mazingira na mamlaka ya kikoloni—hoja inayodhihirika wazi katika kazi za wa Thiong’o zinazoshughulikia unyang’anyi wa ardhi, uharibifu wa mazingira, na kutengwa kwa jamii za vijijini. Vivyo hivyo, dhana ya “slow violence” (vurugu ya polepole) ya Rob Nixon (2011) inatoa mfumo wa kuelewa jinsi wa Thiong’o anavyoonyesha madhara ya polepole lakini yenye athari kubwa ya sera za kikoloni na za baada ya ukoloni, hasa kwa jamii za vijijini. Katika riwaya kama *Petals of Blood* (Petali za Damu, 1977) na *Wizard of the Crow* (Mchawi wa Kunguru, 2006), ardhi haifanyi kazi kama mandhari tu, bali kama kiini cha mapambano ya kisiasa, ikiashiria unyonyaji wa kiuchumi na kupokonywa kwa utamaduni.

Ngũgĩ wa Thiong’o na Maadili ya Uwajibikaji wa Kifasihi

Kiini cha urithi wa kifikra wa Ngũgĩ wa Thiong’o kinapatikana katika dhamira yake thabiti kwa uwajibikaji wa kimaadili. Kwa mtazamo wake, nafasi ya mwandishi haiwezi kutenganishwa na mazingira ya mapambano ya kijamii na kisiasa. Fasihi, kwa maoni yake, si shughuli ya kisanii isiyoegemea upande wowote; daima inahusiana na mahusiano ya mamlaka. Msimamo huu unaendesha kazi zake zote na kumtofautisha na maandishi wanaotafuta kujitenga na siasa kwa kisingizio cha uhuru wa kisanii.

wa Thiong’o anaeleza msimamo huu kwa uwazi zaidi katika *Writers in Politics: Essays* (Waandishi katika Siasa: Insha), ambapo anasisitiza kwamba “the writer has no choice but to align himself with the people, for neutrality in situations of injustice is itself a form of complicity” (mwandishi hana chaguo ila kujiweka upande wa wananchi, kutoegemea upande wowote katika mazingira ya dhuluma ni namna ya kushiriki katika dhuluma hiyo) (1981, uk. 72). Kauli hii inaeleza wazi mtazamo wake kwamba uwajibikaji wa kifasihi ni wajibu wa kimaadili. Kwa mujibu wake, uandishi lazima uwe sehemu ya mapambano ya haki; la sivyo, utakuwa chombo cha kuendeleza ukandamizaji.

Msimamo huu wa kimaadili hauwezi kutenganishwa na msisitizo wake juu ya lugha. Uamuzi wake wa kuacha kutumia Kiingereza kama lugha ya ubunifu haukuwa chaguo la mtindo wa uandishi, bali ulikuwa tendo la kimaadili. Kwa kuandika kwa lugha ya Gĩkuyu, wa Thiong’o alijitambulisha wazi na wale waliotengwa katika nafasi za kifasihi na kitaaluma. Msomi huyu alikataa wazo kwamba umaarufu wa kimataifa unapaswa kupatikana kwa gharama ya uhalisia wa kitamaduni. Kama anavyoeleza, “To choose a language is to choose a way of seeing the world” (Kuchagua lugha ni kuchagua namna ya kuutazama ulimwengu) (wa Thiong’o, 1986a uk. 16).

Aidha, maadili ya uwajibikaji kwa wa Thiong’o yanaenea hadi katika ufafanuzi wake wa hadhira. Tofauti na maandishi wengi wa baada ya ukoloni ambao wasomaji wao wakuu hupatikana katika taasisi za kitaaluma za Magharibi, wa Thiong’o alilenga kuzungumza na watu wa kawaida—wakulima, wafanyakazi, na wanafunzi. Ushiriki wake katika tamthilia za jamii, matumizi yake ya mbinu za simulizi za mdomo, na msisitizo wake juu ya ufikikaji vinaakisi maono ya kidemokrasia ya utamaduni. Katika mtazamo huu, fasihi si mali ya tabaka la wasomi pekee, bali ni mazoezi ya pamoja yanayohusisha jamii nzima.

Zaidi ya hayo, mfumo wake wa kimaadili unapinga kukata tamaa. Hata katika kazi zake zenye ukosoaji mkali zaidi, anaendelea kuthibitisha uwezekano wa upinzani na uhuishaji wa kijamii. Kejeli zake, ingawa ni kali, hazijajengwa juu ya kukata tamaa bali juu ya imani katika uwezo wa mwanadamu kubadilisha hali yake. Mtazamo huu unamtofautisha na mikondo mingine ya nadharia ya ubaada ukoloni inayosisitiza zaidi hali ya kukwama au kukata tamaa, na badala yake unamweka katika mapokeo ya fikra za ukombozi zinazochukulia utamaduni kama eneo la mapambano na matumaini.

Kwa kudumisha msimamo huu katika kipindi cha miongo mingi ya ukandamizaji wa kisiasa, uhamisho, na vikwazo vya kitaaluma, wa Thiong’o anaonyesha uthabiti wa kipekee kati ya fikra na matendo. Maisha yake yanaonyesha kwamba kazi ya kifikra inaweza kubaki na misingi ya kimaadili bila kupoteza undani au ukali wa uchambuzi. Uthabiti huu, labda kuliko kazi yoyote mahususi, ndio unaofafanua urithi wake Ngũgĩ wa Thiong’o.

Hitimisho: Ngũgĩ wa Thiong’o na Mustakabali wa Fikra za Kuondoa Ukoloni

Safari ya kifikra ya Ngũgĩ wa Thiong’o inawakilisha mojawapo ya michango endelevu na yenye kina zaidi katika uchambuzi wa ukoloni na athari zake katika historia ya kisasa. Kuanzia riwaya zake za mwanzo zilizojikita katika uhamasishaji wa kitaifa hadi maandiko yake ya baadaye ya kinadharia, wa Thiong’o ameendelea kwa uthabiti kuchunguza miundo inayojenga utawala, utambulisho, na kumbukumbu za kitamaduni. Msisitizo wake juu ya haki ya lugha, usawa wa maarifa, na uwajibikaji wa kimaadili unaendelea kuwa na umuhimu mkubwa katika mijadala ya kisasa kuhusu kuondoa ukoloni, Pamoja na ukosefu wa usawa wa kimataifa.

Zaidi ya kuwa mwandishi wa fasihi, wa Thiong’o anajitokeza kama mbunifu wa fikra za kuondoa ukoloni ambaye kazi yake inaunganisha fasihi, falsafa, na nadharia ya kisiasa. Urithi wake unawataka wanazuoni kufikiria upya misingi ya uzalishaji wa maarifa, kuhoji ngazi za mamlaka zilizojengwa ndani ya lugha, na kutambua fasihi kama eneo muhimu la upinzani. Katika enzi inayoshuhudia kuongezeka kwa mapambano kuhusu utamaduni, mamlaka, na uhusiano wa kijamii, Ngũgĩ wa Thiong’o anabaki kuwa si tu mwenye umuhimu bali pia asiyeweza kuepukika katika mijadala ya kimataifa.

Marejeo

Alexander, N. (1989). *Language policy and national unity in South Africa/Azania*. Buchu Books.

Cooper, C. (1995). *Noises in the blood: Orality, gender, and the “vulgar” body of Jamaican popular culture*. Duke University Press.

Devonish, H. (1986). *Language and liberation: Creole language politics in the Caribbean*. Karia Press.

Gikandi, S. (2000). *Ngũgĩ wa Thiong’o*. Cambridge University Press.

Huggan, G., & Tiffin, H. (2010). *Postcolonial ecocriticism: Literature, animals, environment*. Routledge.

Mignolo, W. D. (2011). *The darker side of Western modernity: Global futures, decolonial options*. Duke University Press.

Nixon, R. (2011). *Slow violence and the environmentalism of the poor*. Harvard University Press.

Quijano, A. (2000). Coloniality of power, Eurocentrism, and Latin America. *Nepantla: Views from South*, 1(3), 533–580.

Sibanda, B. (2024). *The decolonial politics and philosophy of Ngũgĩ wa Thiong’o*. Lexington Books.

wa Thiong’o, N. (1964). *Weep not, child*. Heinemann.

wa Thiong’o, N. (1965). *The river between*. Heinemann.

- wa Thiong’o, N. (1967). *A grain of wheat*. Heinemann.
- wa Thiong’o, N. (1977). *Petals of blood*. Heinemann.
- wa Thiong’o, N. (1980). *Devil on the cross*. Heinemann.
- wa Thiong’o, N. (1981). *Writers in politics: Essays*. Heinemann.
- wa Thiong’o, N. (1986a). *Decolonising the mind: The politics of language in African literature*. Heinemann.
- wa Thiong’o, N. (1986b). *Matigari*. Heinemann.
- wa Thiong’o, N. (1993). *Moving the centre: The struggle for cultural freedoms*. Heinemann.
- wa Thiong’o, N. (2006). *Wizard of the crow*. The New Press.
- wa Thiong’o, N. (2010). *Dreams in a time of war: A childhood memoir*. Pantheon Books.
- wa Thiong’o, N. (2012). *Globalectics: Theory and the politics of knowing*. Columbia University Press.

Kuhusu Mwandishi

Dkt. Paul M. Mukundi ni Profesa Msaidizi wa Kiingereza na Fasihi ya Kiafrika na ya Waasili wa Afrika Ughaibuni katika Chuo Kikuu cha Morgan (Morgan State University), Baltimore, Maryland. Alipata shahada ya B.Ed. (Honors) katika Kiingereza na Fasihi ya Kiafrika kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta (Kenyatta University), Nairobi, Kenya, na shahada zake za uzamili (M.A. katika Kiingereza) pamoja na uzamivu (Ph.D. katika Kiingereza na Fasihi ya Baada ya Ukoloni) kutoka Chuo Kikuu cha Morgan. Kwa takribani miaka ishirini, amehudumu kama mhadhiri na msimamizi wa kitaaluma katika vyuo vikuu nchini Marekani—ikiwemo Morgan State University, Coppin State University, na Virginia Union University—na pia nchini Kenya katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, ambako alihudumu kama Mratibu wa Programu za Uzamili katika Fasihi ya Kiingereza na baadaye kama Mkurugenzi wa Programu ya Uongozi chuoni humo. Amehudhuria na kutoa mada katika mikutano ya kitaaluma nchini Marekani, Kanada, Kenya, Senegal, na Afrika Kusini. Vile vile, makala pamoja na sura za vitabu vyake zimechapishwa katika machapisho mbalimbali. Yeye ndiye mwandishi wa *Preventing Things from Falling Further Apart: The Preservation of Cultural Identities in Postcolonial African, Indian, and Caribbean Literatures* (Kuzuia Mambo Yasivunjike Zaidi: Uhifadhi wa Utambulisho wa Kitamaduni katika Fasihi za Baada ya Ukoloni za Kiafrika, Kihindi, na Karibiani, 2010).

About the Author

Dr. Paul M. Mukundi is Assistant Professor of English and African and African Diasporic Literature at Morgan State University, Baltimore, Maryland. He earned his B.Ed. (Honors) degree in English and African Literature from Kenyatta University, Nairobi, Kenya, and his M.A. (English) and Ph.D. (English and Postcolonial Literature) from Morgan State University. For close to twenty years, he has served as university instructor and administrator in the USA—including at Morgan State University, at Coppin State University, and at Virginia Union University—and in Kenya, at Kenyatta University, where he served as Coordinator of Graduate Programs in English Literature and later as Director of the campus-wide Leadership Program. He has

spoken in academic conferences in the USA, Canada, Kenya, Senegal, and South Africa, and his articles and book chapters have featured in many publications. He is the author of *Preventing Things from Falling Further Apart: The Preservation of Cultural Identities in Postcolonial African, Indian, and Caribbean Literatures* (2010).

Recebido em: 03/2026

Aceito em: 30/07/2026

Para citar este texto (ABNT): MUKUNDI, Paul M. Kumkumbuka Ngũgĩ wa Thiong’o: Shujaa wa Kifikra na Fasihi Kutoka Afrika. *Njinga & Sepé: Revista Internacional de Culturas, Línguas Africanas e Brasileiras*. São Francisco do Conde (BA), vol.6, nº Especial II, p.313-326, agosto 2026.

To cite this text (APA): Mukundi, Paul M. (august 2026). Kumkumbuka Ngũgĩ wa Thiong’o: Shujaa wa Kifikra na Fasihi Kutoka Afrika. *Njinga & Sepé: Revista Internacional de Culturas, Línguas Africanas e Brasileiras*. São Francisco do Conde (BA), 6 (Special II): 313-326.